

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



Unapojibutafadhalitaja:

Tarehe: 08 Januari, 2023

## TAARIFA KWA UMMA

Mnamo tarehe 08.01.2023 zilisambazwa taarifa za kupotosha kuitia mitando ya kijamii kuwa, Shule ya Msingi Twiga iliyopo Kata ya Wazo, Manispaa ya Kinondoni, imefanya matumizi mabaya ya fedha kiasi cha shilingi 29,000,000.00 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa choo chenye matundu 12, chemba Mbili zenyne upana na urefu wa mita 12 kwa futi 10, bati 50 za geji 30, tofali 2,000, saruji nondo na vifaa vingine vya ujenzi.


Tunapenda kuutarifu umma kuwa, taarifa hizo si za kweli kutokana na ukweli kuwa; Mnamo 17.10.2022 Mkurugenzi wa Manispaa kuitia kikao cha Menejiment (CMT) aliagiza kufanyika kwa ukaguzi maalum wa ujenzi wa matundu hayo ya vyoo. Kufuatia agizo hilo, Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa kuitia ukaguzi huo maalum alibainisha yafuatayo:

1. Kutokana na Jiografia ya eneo hilo, mradi huo ili ukamilike kwa mujibu wa BoQ, ilitengewa kiasi cha shilingi 32,359,010.00 na hadi tarehe ya ukaguzi huo mradi ulikuwa umepokea jumla ya shilingi 29,000,000.00.
2. Jumla ya shilingi 26,571,884 zilikuwa zimetumika na shilingi 2,428,116 zilikuwa bado zimo kwenye akaunti ya shule.
3. Matundu ya choo yanayojengwa ni 13 na si 12 kama taarifa hiyo ilivytuhumu.
4. Vifaa vya ujenzi vilivytumika hadi hatua hiyo ya mradi wakati unakaguliwa vilikuwa ni bati za geji 28 na siyo geji 30.

Kutokana na maoni ya Mkaguzi kupendekeza kuwa zitafutwe fedha nyingine kwa ajili ya ukamilishaji, mnamo tarehe 06.01.2023 mchakato ulifanyika kuitia vikao halali, ambapo mradi huo tayari umetengewa fedha (kuitia re-allocation) ili umaliziaji ufanyike ambapo kazi zilizobaki ni uwekaji wa tiles, kununua madirisha na kuweka mifumo ya maji taka na maji safi..

Tunawaomba radhi wale wote walioguswa na taarifa hiyo potofu na kwamba iwapo Mwananchi una dukuduku lolote kuhusu utekelezaji wa miradi ya Manispaa, tafadhalii usisite kufika Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ili kupata ufanuzi sahihi.

Imetolewa na:



Aquilinus Shiduki

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano

Manispaa ya Kinondoni.

08.01.2023